

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI
IDARA YA UHAMIAJI

ANUANI YA SIMU: "UHAMIAJI"
TELEFAX: +255 26 2323532
SIMU +255 26 2323542
+255 26 2323543



OFISI YA KAMISHNA JENERALI WA
UHAMIAJI
4 BARABARA YA MWANGOSI,
UZUNGUNI,
S. L. P 1181,
DODOMA.

02 Oktoba, 2021

TANGAZO LA AJIRA

Kamishna Jenerali wa Uhamiaji anatangaza nafasi za ajira tano (5) za cheo cha Konstebo wa Uhamiaji kwa vijana waliohitimu shahada katika fani ya *Civil Engineering* (nafasi tatu) na *Mechanical Engineering* (nafasi mbili) ambao wamefuzu Mafunzo mbalimbali ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) au Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) waliopo Makambini au waliohitimu mafunzo hayo na wenye sifa zifuatazo:-

- i. Awe raia wa Tanzania mwenye umri usiopungua miaka 22 na usiozidi miaka 30.
- ii. Awe na tabia njema, asiwe amewahi kufungwa, au kujihusisha na matumizi au biashara ya dawa za kulevywa, au uhalifu wa aina yoyote.
- iii. Asiwe na alama yoyote au michoro katika mwili wake.
- iv. Asiwe amejiriwa/hajawahi kuajiriwa Serikalini.
- v. Awe tayari kuhudhuria Mafunzo ya awali ya Uhamiaji.
- vi. Awe tayari kufanya kazi mahali popote nchini Tanzania.
- vii. Awe na afya njema ya mwili na akili, na aambatishe Taarifa ya Daktari kutoka katika Hospitali yoyote ya Serikali.
- viii. Awe na ujuzi wa Kompyuta.
- ix. ***Uzoefu wa kazi usiopungua miaka miwili.***

2. Namna ya kufanya Maombi:

Muombaji anatakiwa kuandika barua ya Maombi ya ajira kwa mkono wake akiambatisha nyaraka zifuatazo:-

- i. Barua ya Utambulisho toka Serikali ya Mtaa/Kijiji au Shehia,
- ii. Kwa waombaji waliopo Makambini, barua zao zipitie kwa Wakuu wa Kambi husika,
- iii. Nakala ya Cheti cha Kuzaliwa,
- iv. Namba au Kitambulisho cha Taifa (NIDA) au Kitambulisho cha Mzanzibari,
- v. Vyeti vya kuhitimu shule (Leaving Certificates),
- vi. Vyeti vya Taaluma (Academic Certificates),
- vii. Wasifu wa Mwombaji (CV),
- viii. Picha Nne (04) za Pasipoti zenye rangi ya Bluu.

3. Maombi yatumwe kupitia anuani ifuatayo;

KAMISHNA JENERALI WA UHAMIAJI,
UHAMIAJI MAKAO MAKUU,
S. L. P. 1181,
DODOMA

4. Mwisho wa kuwasilisha maombi ni tarehe 16 Oktoba, 2021.

5. Tahadhari;

Ikumbukwe kuwa Mwombaji yoyote atakayebainika kuwasilisha nyaraka za kughushi atachukuliwa hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na kufikishwa Mahakamani.

Limetolewa na,

SI - PAUL MELLE
MSEMAJI MKUU WA UHAMIAJI
MAKAO MAKUU - DODOMA
02 Oktoba, 2021